

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**  
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)**

Tel. 025-2530404

FAX NO. 025-253023



S.L.P 73,  
**TUNDUMA.**  
**SONGWE- TANZANIA.**

21/ 05/2021

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma anawatangazia wananchi wenye sifa nafasi za Ajira ya mkataba kwa kazi ya Wafanya usafi katika Hospitali ya Mji Tunduma.

**WATUNZA KUMBUKUMBU NAFASI 4**

**Sifa za mwombaji**

- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe Stashahada ya utunzaji wa kumbukumbu kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Awe na uzoefu wa utunzaji wa kumbukumbu za matibabu/Afya.
- iv. Awe na umri wa kuanzia miaka 18-45.
- v. Aambatanishe picha za rangi mbili (passport size)

**Kazi na majukumu**

- i. Kutunza kumbukumbu za kimatibabu kitengo cha mapokezi.
- ii. Kuandikisha wagonjwa kitengo cha mapokezi.
- iii. Kuandaa taarifa takwimu za wagonjwa wa nje na wakulazwa wanaotibiwa katika vitengo vyote.
- iv. Kuhifadhi takwimu za wagonjwa wote walioruhusiwa kwa matumizi ya baadae.
- v. Kusimamia huuishwaji wa mifumo yote ya taarifa.
- vi. Kuhifadhi stakabadhi za malipo ya wagonjwa.
- vii. Na majukumu mengine utakayopangiwa na Mkuu wako wa kazi.

**WAFANYA USAFI NAFASI 10**

**Sifa za mwombaji**


- i. Awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe anajua kusoma na kuandika

- iii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18-45.
- iv. Awe na akili timamu

**Kazi na majukumu**

- i. Kufanya usafi maeneo yote ya Hospitali ya Mji.
- ii. Kutoa elimu ya usafi wa mazingira.
- iii. Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa bila kuchafuliwa.
- iv. Kutunza na kuhifadhi vifaa vya kufanyia usafi.

Mwisho wa Kutuma Maombi ni tarehe 28/05/2021 saa 9:30 Alasiri



**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**Maombi yote yatumwe kwa:-**

Mkurugenzi wa Mji  
Halmashauri ya Mji  
S.L.P 73  
**TUNDUMA**